

Learning by Ear 2010  
Series: 'Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace'  
Episode: 05 Kassi and Kaloo  
Author: Ibrahima Ndiaye

**LEARNING BY EAR 2010**  
**SHALL I TELL YOU SOMETHING?**  
**AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE**

**EPISODE 05: "KASSI AND KALOO"**

**AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE**  
**EDITOR: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,  
NAÏMA GUIRA**  
**TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS**  
**PROOFREADING: TONY DUNHAM**

**KISUAHELI: ERIC PONDA**

***Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor***

**CHARACTERS:**

1. NARRATOR (female, 40 years old at least)
2. KING KATONGO (male, 30 years old at least)
3. WEAVER BIRD (female, about 20 years old)
  
4. KASSI THE HORSE (male, about 20 years old)
5. KALOO THE HORSE (male, about 20 years old)
6. Two or three GUARDS (male, age irrelevant)

## **INTRO / PRESENTER:**

Hujambo na karibu kwa makala ya tano kwenye mfululizo huu wa ngano zetu “Je Nikudokezee”, ngano za jamii ya Mwafrika kuhusu mbinu za kudumisha amani na maridhiano miongoni mwao. Bila shaka umewahi kushawishiwa kufanya jambo ambalo unaona ni makosa kwa kauli yako. Na hasa wakati ambapo anayefanya hivyo ni mtu mwenye uwezo na mamlaka juu yako ambaye huwezi kumkatalia jambo. Ndio maada yetu leo, nikitaraji utaendelea kuwa nasi hadi mwisho wa ngano hii ya Kassi na Kaloo ili ufahamu kwanini ndugu ni kufaana na wala sio kufanana.

### **1. MUSIC (*play as background for the entire script*)**

### **2. NARRATOR:**

Siku hiyo kulikuwa na joto sana ingawa upepo mzuri ulikuwa ukivuma kutoka baharini.

### **3. SFX: *Light breeze blows***

### **4. NARRATOR:**

Ni katika ukanda wa Savana kuliko na himaya ya Babakadi ya Mfalme Katongo Bisso na Bisso aliyeogopewa sana. Jina la Bisso na Bisso lilimaanisha mtu mwenye kuwanyanyasa na kuwadhulumu wengine. Mfalme huyo aliogopewa sana na watu wake. Punde tu

alipochukua usukani, Mfalme Bisso na Bisso alijenga jeshi lililomzunguka lililoogopewa sana ndani na nje ya mipaka ya ufalme huo wa Babakadi na alipenda sana farasi.

**5. SFX: *Neighing horses***

**6. NARRATOR:**

Mfalme Katongo aliwapenda sana wanyama hawa na hakuna jambo ambalo lingeweza kumzuia kumpata farasi aliyependa iwe mahali popote pale. Siku moja alisikia habari za Mfalme Baye Fall wa Ndambour, aliyekuwa akifuga farasi wengi sana. Kila mwaka, walizaliwa farasi wa kupendeza sana katika makao yake. Na mwaka huo wanafarasi wawili wakupendeza wasio na mfano wakazaliwa, mmoja mweusi tii aliyepewa jina la Kassi na mwengine mweupe kama pamba aliyepewa jina la Kaloo. Farasi hawa walikulia pamoja na kupendana sana, ilikuwa vigumu kuwatenganisha. Na Mfalme Katongo aliposikia habari hizo siku moja akawaita walinzi wake.

**7. King KATONGO:**

“Hebu mtayarisheni farasi wangu nataka kwenda kukutana na Baye Fall maana nimewapenda wanafarasi wake wawili na Baye Fall lazima anipe mara moja...! Kisha fanyeni upesi!”

**8. 2-3 Guards:**

“Sawa Mfalme!”

**9. SFX: *Sentinels run away (played by actors)***

**10. NARRATOR:**

Na hapo walinzi wakatii amri na kutekeleza maagizo hayo mara moja. Hao wakafunga safari hadi kwa Mfalme Baye Fall. Hata hivyo Mfalme Baye Fall hakuwa mwepesi wa kukubali ombi la kuwatoa wanafarasi wake. Lakini baada ya mashauriano ya muda mrefu akakubali kumuuzia Mfalme Katongo yule mwanafarasi mweupe Kaloo. Hata hivyo Mfalme Katongo hakutosheka, aliendelea kumtamani yule mwanafarasi mweusi Kassi. Lakini Baye Fall akakataa kata kata. Hii ilimkasirisha sana Mfalme Katongo ambaye alihisi kudharauliwa. Na mara moja akatangaza vita dhidi ya Baye Fall.

**11. SFX: *Neighing horses, Kassi & Kaloo***

**12. NARRATOR:**

Mfalme Katongo alianza kuwaandaa wanajeshi wake kwenda vitani. Farasi Kaloo, aliyempenda sana ndiye aliyekuwa wa kwanza kutayarishwa. Kwa upande wake Mfalme Baye Fall pia akamuandaa Farasi Kaasi tayari kupambana na Mfalme Katongo. Pande hizo mbili zikakutana katika eneo wazi kabisa mfano wa jangwa.

**13. SFX: *War sounds: whistling arrows, gunshots, horses neighing loudly, men shouting***

**14. SFX: KASSI & KALOO: *Neighing horses***

**15. NARRATOR:**

Ama kwa hakika vilikuwa vita vya kufa kuona. Mfalme Katongo juu ya farasi Kaloo akiwa amezungukwa na wanajeshi wake huku naye Mfalme Baye Fall akimtumia farasi Kassi. Wapiganaji hao

walishambuliana vikali kwa kutumia mishale yenye sumu. Milio ya risasi, farasi na makelele ya wapiganaji vilitawala anga ya eneo hilo la mapigano. Na mapigano hayo yakadumu kwa muda mrefu licha ya watu wengi kuuwawa kutoka pande zote mbili.

Baada ya siku kadhaa za mapigano, Mfalme Katongo bado akiwa juu ya Farasi Kaloo, alimtahadharisha vikali adui yake Baye Fall ambaye pia alikuwa juu ya farasi Kasi.

**16. KATONGO:**

“Baye Fall, kama hutanipa huyo farasi wako, nitakuua. Mbona unakaidi amri ya mfalme wa Babakadi?”

**17. NARRATOR:**

Wakati wafalme hao wakijibizana, farasi hawa Kaloo na Kasii walionana uso kwa uso. Wakaangaliana kwa hasira, wakisahau kabisa kwamba walizaliwa na kuishi katika zizi moja. Kwa hakika uhasama wao ulikuwa umechochewa na chuki baina ya wafalme wao. Wakapambana vikali.

**18. KASSI & KALOO: *Fight between two horses***

**19. NARRATOR:**

Farasi hao walirukina kwa hasira na kupigana mieleka kwenye tope mbele ya wafalme wao. Baada ya mapigano ya muda mrefu, Kassi na Kaloo walianza kutokwa na damu kwenye pua, midomo na kila mahali, lakini hakuna aliyetaka kusalimu amri. Mara kwa mara walipumzika na kisha kurejelea mapigano. Maskini laiti wangepahamu enzi zao za utotoni wakiishi zizi moja, kucheza pamoja na utukutu wa kutoroka mara kwa mara kwenda vichakani, kwa hakika hawangepigana mieleka! Na kadri walivyoendelea

kupigana ndivyo hasira zilivyowapanda, hadi wakaanguka kama mbuyu na wakazimia huku wakiwa wamelaliana!

**20. KASSI & KALOO: Horses neighing exhaustedly**

**21. NARRATOR:**

Kwa jinsi walivyopigana, ungedhani farasi hao walitoka wakati wa vita vya pili vya dunia. Kassi na Kaloo walilala chini kwa maumivi huku damu zikiwatoka. Asubuhi, walipokuwa bado wamelaliana pale chini, ndege mnana akiwa katika pita pita zake akawaona na kisha akatua katika mbuyu mmoja kuhafamu zaidi kilichokuwa kikiendelea. Maiti na mizoga ya wanyama ilitapakaa kila mahali katika eneo hilo huku mishale, maganda ya risasi na damu vikidhihirisha vita vikali vilivyoendelea mahali hapo. Tayari nzi akifuatiwa na fisi walikuwa wamefika kusherehekea mizoga. Kwarara nao ambao hupenda sana kula nzi pia walifika mahala hapo kuwawinda nzi walafi waliokuwa wakijishibisha kutokana na damu ya farasi hao wawili. Kwa kuwa ndege mnana alikuwa na hamu ya kujua kilichotokea akajaribu kuwaamsha farasi wawili.

**22. WEAVER BIRD chirping**

**23. WEAVER BIRD**

“Simameni mnieleze kichotokea hapa. Mbona kuna damu iliyotapakaa kila mahali hapa? Nini balaa hii yote?”

**24. KASSI beginning & KALOO finishing the sentence**

“Wafalme wetu walianza kupigana...na sisi tukajikuta katikati ya

mapigano hayo.”

**25. WEAVER BIRD**

“Samahani hebu ngojeni kidogo! Kwani vita vya binadamu hawa vinawahusu nini nyinyi hayawani? Waacheni wapigane vita vyao kama hawana la kufanya. Kwani ninyi hamna akili kuingizwa katika vita visivyowahusu?”

**26. KALOO**

“Ni kweli unayosema! Lakini sisi tunatii amri za wafalme wetu! Na wao hawatujali hata kidogo, sisi si muhimu kwao.”

**27. WEAVER BIRD**

“Ujinga gani! Ninyi ni wamoja! Yaani unaweza kujitosa kwenye ziwa lililojaa mamba eti kwa sababu Mfalme amekuamrisha? Kwani huna akili? Hii ni aibu kubwa kwa sababu mnastahili kuwa marafiki badala ya kupigana.

**28. NARRATOR:**

Maneno haya yaliwafanya farasi hao kuangaliana tena mara mbili mbili na kisha kuinamisha vichwa vyao chini kwa huzuni huku wakijilaumu kwa kuumizana pasi na sababu yoyote. Na baada ya kimya cha muda mrefu Kassi akamwambia farasi mweupe.

**29. KASSI:**

“Wewe si Kaloo?”

**30. KALOO (*in tears*):**

“Na wewe si Kassi?”

**31. NARRATOR:**

Hatimaye fahamu zikawajia. Kwa kuona aibu, walijipangusa vumbi na kuinuka tena. Licha ya maumivu waliokuwa nayo, walikumbatiana kwa furaha kwani hawakuwa wameonana kwa muda mrefu sana! Ndege mnana pia alikuwa na furaha kuwapatanisha na kusema:

### **32. WEAVER BIRD**

*(Talking to herself in a low voice)*

“Ah, nimefaulu! Na wala hata haikuwa kazi kubwa. Labda kuanzia sasa naweza kuchukulia taaluma hii ya upatanishi. Viumbe ni waajabu sana kwani hawawezi kuona ukweli hata ukiwa osoni mwao. Kazi hii inaweza kuwa nzuri sana na yenye kuniletea pato kubwa kushinda kuuza minyoo na konokono sokoni.

*(Aloud to the horses)*

Kwa hivyo mnafahamiana! Bora niwaache sasa maana kazi yangu inanisubiri. Nawatakia kila la kheri maishani.”

### **33. WEAVER BIRD *chirps and flies away***

### **34. NARRATOR**

Baada yandeghe kuondoka, Kassi alikuwa wa kwanza kuzungumza.

### **35. KASSI**

“Kaloo, sisi tumekuwa kama vipofu! Hakukuwa na haja kwamwe kujihusha na na vita hii. Hakuna kitu kibaya kama vita. Hebu sasa tazama hali tuliyo!”

### 36. KALOO

“Kassi, hebu twende. Kuanzia leo tutaishi pamoja tena.”

### 37. SFX: Horses trotting

### 38. NARRATOR:

Kassi na Kaloo wakaandamana na kuanza kuishi pamoja tena. Na hadi sasa bado wanaishi pamoja.

*Na hadi hapo ngano yetu imefika ukingoni na wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu..*

### 39. Music

#### OUTRO:

Labda siku moja umejikuta katika hali hii, kutekeleza maagizo ambayo ni kinyume kabisa na matakwa yako. Iwapo yamekukuta, basi yasimulie wenzako au tuandikie barua pepe kupitia anuani hii [lbe@dw-world.de](mailto:lbe@dw-world.de).

Na endapo ungependa kusikiliza tena kipindi hiki au vingine vya Noa Bingo, tembelea mtandao wetu wa [www.dw-world.de](http://www.dw-world.de) Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.!

END